

TANGAZO LA SERIKALI NA. 408 la tarehe 24/5/2024

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
SURA 415

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(1))

NOTISI YA UTEUZI WA WAENDESHA MASHTAKA ZA MWAKA 2024

- Jina
- TS Na.
384 la 2023
- Marekebisho
ya kifungu
wezeshi
- Marekebisho
ya kanuni ya 4
- Kupanga upya
kanuni ya 4
1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji za Mwaka 2024, na zitasomwa pamoja na Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji za Mwaka 2023 ambazo katika Kanuni hizi zitarejewa kama “Kanuni kuu”.
 2. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuvifuta vifungu wezeshi na badala yake kuweka kifuatacho:
“(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(1))”
 3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 4:
 - (a) katika kanuni ndogo ya (2)(a) kwa-
 - (i) kuweka neno “na” mara baada ya aya ndogo ya (ii);
 - (ii) kufuta nukta mkato “;” na neno “na” yaliyopo katika aya ndogo ya (iii) na badala yake kuweka nukta “.”; na
 - (iii) kufuta aya ndogo ya (iv); na
 - (b) katika kanuni ndogo ya (2)(b) kwa-
 - (i) kuweka neno “na” mara baada ya aya ndogo ya (ii);
 - (ii) kufuta nukta mkato “;” na neno “na” yaliyopo katika aya ndogo ya (iii) na badala yake kuweka nukta “.”; na
 - (iii) kufuta aya ndogo ya (iv);
 4. Kwa kupanga upya kanuni ya “4” iliyojirudia

yenye maelezo ya pembeni “Maombi ya usajili” na maudhui yake kama kanuni "5".

Marekebisho
ya kanuni ya 6

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6 :
- (a) katika kanuni ndogo ya (2), kwa kufuta neno “linaweza” na badala yake kuweka neno “litatoa”; na
 - (b) katika kanuni ya (3), kwa kuweka maneno “ndani ya siku saba za kazi kuanzia tarehe ya kupokea maombi” katikati ya maneno “Shirika” na “litatoa”.

Marekebisho
ya kanuni ya
11

6. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 11(1)(b) kwa kufuta maneno “na nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na Shirika”.

Marekebisho
katika Jedwali
la Kwanza,
Pili, Tatu,
Nne, Tano,
Sita na Saba

7. Kanuni kuu zinarekebishwa kwenye Majedwali kwa kufuta kanuni wezeshi katika:
- (a) Jedwali la Kwanza na badala yake kuweka ifuatayo:
“(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5, 11(1) na 12(1)(a))”;
 - (b) Jedwali la Pili na badala yake kuweka ifuatayo:
“(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5, 11(1) na 12(1)(c))”;
 - (c) Jedwali la Tatu na badala yake kuweka ifuatayo:
“(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(2) na 12(c))”;
 - (d) Jedwali la Nne na badala yake kuweka ifuatayo:
“(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(3))”;
 - (e) Jedwali la Tano na badala yake kuweka ifuatayo:
“(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(1))”;

(f) Jedwali la Sita na badala yake kuweka ifuatayo:

“(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 13(1))”; na

(g) Jedwali la Saba na badala yake kuweka ifuatayo:

“(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19 na 20(1))”.

Dodoma,
3 Mei, 2024

MAKAME M. MBARAWA
Waziri wa Uchukuzi